

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

## PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com



## MATANGAZO - DOMINIKA YA 4 YA MAJILIO MWAKA A - 21.12.2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | LEO DOMINIKA<br>21.12.2025 | **DOMINIKA YA 4 YA MAJILIO**<br>*Mchango wa Pili ni kwa ajili ya Holly Childhood* |
| 2. | JUMATANO<br>24.12.2025 | Misa ya Mkesha wa Noeli<br>Muda 3:00 usiku<br>Wasimamizi: UWAKA |
| 3. | ALHAMISI<br>25.12.2025 | **SHEREHE YA KUZALIWA BWANA - NOELI**<br>**Misa ya 1: Saa 1:00 asubuhi**<br>Wasimamizi: WAWATA<br>Watangaza Neno:<br><br>**Misa ya 2: Saa 3:00 asubuhi**<br>Wasimamizi: VIWAWA<br>Watangaza Neno: |
| 4. | IJUMAA<br>26.12.2025 | Kumbukumbu: Sikukuu ya Mt. Stefano Shahidi<br>**Misa ni 1 tu saa 2:00 asubuhi** |
| 5. | JUMAMOSI<br>27.12.2025 | Sikukuu ya Mt. Yohane Mtume na Mwinjili<br>Kutakuwa na Misa katika Jumuiya ya Mt. Yohane Mtume na Mwinjili saa 1:00 asubuhi<br>**Beach Mass - Misa ya Ufukweni ya Vijana** |
| 6. | JUMAPILI<br>28.12.2025 | **SHEREHE YA FAMILIA TAKATIFU YA YESU, MARIA NA JOSEPH**<br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Familia Takatifu<br>Watangaza Neno: Mary Nyaki na Zawadi Jackson<br><br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Martin De Pores<br>Watangaza Neno: Angela Komba na Hans Kahumba<br><br>**Misa ya 3: Watoto**<br>Wasimamizi: Familia Takaitfu na Mt. Martin De Pores<br><br>*Mchango wa Pili ni kwa ajili ya Ujenzi* |
| 7. | WALEZI WA UTOTO MTAKATIFU | Jumuiya ambazo bado zinakumbushwa kuchagua walezi wawili, mwanamme na mwanamke kuwa walezi wa Utoto Mtakatifu, pia uchaguzi wa viongozi wa Utoto Mtakatifu na orodha ya watoto |

CS CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| | | wanaoshiriki *Sunday School* na Misa ya watoto. |
| 8. | MISA YA WATOTO MASHAHIDI | Misa ya Watoto Mashahidi itafanyika katika Parokia ya Kristo Mfalme Tabata Jumamosi 27.12.2025 saa 3:00 asubuhi. Mchango wa chakula na huduma Jimboni kwa kila mshiriki ni Shs. 15,500. Mwisho wa kutoa ni 24.12.2025 |
| 9. | BAHASHA ZA MARAFIKI WA UINJILISHAJI WA PAPA | Mwisho wa kurejesha Bahasha za Marafiki wa Mashirika ya Uinjilishaji ya Baba Mtakatifu (PMS) ilikuwa ni Dominika iliyopita 30.11.2025. Jumuiya ambazo hazijarejesha bahasha hizo zinatakiwa kurejesha bahasha hizo leo hata kama hazina mchango uliowekwa. Zinatakiwa Baraza la Maaskofu. |
| 10. | VIWAWA | Misa y ufukweni (Beach Mass) ya VIWAWA itafanyika 26.12.2025. Nauli kwa kila kijana ni shs. 10,000. Kila Jumuiya inaombwa kulipia walau vijana 3. Safari itaanza saa 1:00 asubuhi. |
| 11. | BAHASHA ZA RADIO MARIA | Matembezi ya Sanamu ya Bikira Maria yametamatika rasmi wiki jana hapa Parokiani sambamba na kampeni ya Kapu la Mama Maria. Wote waliochukua bahasha na bado hawajarejesha wanaombwa kurejesha leo hata kama hazina mchango. Bado bahasha 208. |
| 12. | UTOTO MTAKATIFU | Mafungo na maungamo kwa watoto wote yatafanyika Jumanne 23.12.2025 kuanzia saa 3:00 asubuhi |
| 13. | MAFUNGO YA NOELI | Mafungo na tafakari ya Majilio kwa ajili ya kujiandaa na Noeli kwa watu wazima yalifanyika jana Jumamosi 20.12.2025 kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka 7:00 mchana ikihusisha mada kuhusu vijana kujitambua katika dunia ya le na pia maungamo. Jumla ya waamini 70 waliohudhuria |
| 14. | UBATIZO WA WATOTO NOELI | Semina ya wazazi na wasimamizi itafanyika Jumanne 23.12.2025 saa 9:00 alasiri. Ubatizo utafanyika katika Misa ya 26.12.2025 saa 2:00 asubuhi |
| 15. | MAHITAJI KWA WAHITAJI NOELI | Waamini wote wanaalikwa kutoa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya wahitaji kwa kipindi cha Noeli kam nguo na vyakula, sabuni, n.k. Vyakula vinavyoharibika haraka kama nyama  viletwe asubuhi siku ya 24.12.2025. Navyo vitagawiwa kuanzia saa 5:00 asubuhi. |
| 16. | USAFI NA MAPAMBO | Waamini wote wanatakiwa kufika Parokiani kwa ajili ya kufanya usafi na mapambo ya Kanisa, Jumatano 24.12.2025 saa 1:30 asubuhi |
| 17. | GAZETI LA TUMAINI LETU | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

***Kauli Mbiu ya Mwaka wa Jubilei Kuu: "Jubilei 2025 – Mahujaji wa Matumaini."***

**TANGAZO LA DARAJA YA UPADRE KWA MARA YA KWANZA**

CS CamScanner

1. Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap wa Jimbo Kuu la DSM anatangaza **Daraja ya Upadri** wa Shemasi **Yohannes Gerald Mfingile C.PP.S** wa Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ( The Society of the Precious Blood) anayefanya mazoezi ya kichungaji katika Parokia ya Mt. Nicholaus, Kunduchi katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam, anayetarajiwa kupewa Daraja Takatifu ya Upadri tarehe 24.01.2026 katika Kanisa la Mwenyeheri Bhakanja, Parokia ya Boko, Jimbo la Bagamoyo.

2. Mhashamu Sana Askofu Mkuu Jude Thaddeus Ruwa'ichi OFMCap wa Jimbo Kuu la DSM anatangaza **Daraja ya Upadri** wa Shemasi **Edson Mwoleka CSC** wa Shirika la Wamisionari wa Msalaba Mtakatifu ( Congregation of the Holy Cross) anatoka katika Parokia ya Roho Mtakatifu - Kitunda, Jimbo Kuu la Dar es Salaam, anayetarajiwa kupewa Daraja Takatifu ya Upadri tarehe 18.01.2026 katika Kanisa la Moyo Mtakatifu wa Yesu, Parokia ya Sombetini, Jimbo Kuu la Arusha.

**MASOMO DOMINIKA – SHEREHE YA FAMILIA TAKATIFU - 28.12.2025**

| | |
|---|---|
| SOMO I | Ybs 3:2-6, 12-14 |
| WIMBO WA KATIKATI | Zab 128:1-5 |
| SOMO II | Kol. 3:12-21 |
| SHANGILIO | Kol 3:15,16 |
| INJILI | Mt 2:13-15, 19-23 |

CS CamScanner